



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA  
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

REF. PSLE 2022



RATIBA YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI  
(PRIMARY SCHOOL LEAVING EXAMINATION TIMETABLE)  
OKTOBA, 2022

TAREHE NA SIKU	MUDA (SAA)	NAMBA MFICHO	SOMO
05.10.2022 JUMATANO	2:00 – 3:40	02	ENGLISH LANGUAGE
	3:40 – 4:30		MAPUMZIKO
	4:30 – 6:30	04 04E	HISABATI MATHEMATICS
	6:30 – 8:30		MAPUMZIKO
	8:30 – 10:00	06 06E	URAI NA MAADILI CIVIC AND MORAL EDUCATION

<b>06.10.2022 ALHAMISI</b>	2:00 – 3:40	01	KISWAHILI
	<b>3:40 – 4:30</b>		<b>MAPUMZIKO</b>
	4:30 – 6:00	05 05E	SAYANSI NA TEKNOLOJIA SCIENCE AND TECHNOLOGY
	<b>6:00 – 8:00</b>		<b>MAPUMZIKO</b>
	8:00 – 9:30	03 03E	MAARIFA YA JAMII NA STADI ZA KAZI SOCIAL STUDIES AND VOCATIONAL SKILLS

## MAELEKEZO MUHIMU

1. Hakikisha kuwa unayo **Ratiba ya Mtihani ya mwaka 2022** iliyoandaliwa na Baraza la Mitihani la Tanzania.
2. **Kabla ya kufungua bahasha** yoyote yenye maswali ya mtihani, hakikisha kwamba **unasoma jina la somo juu ya bahasha husika** na kujihakikishia kuwa somo hilo ndilo linalostahili kufanyika wakati huo kulingana na **Ratiba ya Mtihani**.
3. Endapo utata utajitokeza kati ya **maelekezo yaliyomo ndani ya Karatasi ya Mtihani** na **Ratiba ya Mtihani**, **maelekezo yaliyomo katika karatasi ya Mtihani husika ndiyo yatakayofuatwa**.
4. Watahiniwa wenye mahitaji Maalum (**Wasioona, Uoni Hafifu, Viziwi**) waongezewe **MUDA WA ZIADA WA DAKIKA 20 KWA KILA SAA** kwa somo la **Hisabati na DAKIKA 10 KWA KILA SAA** kwa masomo mengine.
5. Msimamizi wa Watahiniwa **WASIOONA** awe mtaalamu aliye na **uwezo wa kusoma maandishi na alama za 'Braille'** na Msimamizi wa Viziwi awe ni mtaalamu aliye na uwezo wa lugha ya alama.
6. Watahiniwa wenye **UONI HAFIFU** wapewe karatasi za mtihani na za kujibia zenye **maandishi yaliyokuzwa**, zilizoandaliwa na Baraza la Mitihani la Tanzania kwa matumizi yao.
7. Karatasi zenye majibu ya watahiniwa wenye **UONI HAFIFU** zifungwe kwenye **bahasha za pekee**. Zisichanganywe na karatasi za watahiniwa wenye Uoni wa kawaida.
8. Watahiniwa waelekezwe;
  - (a) Kuingia ndani ya chumba cha Mtihani nusu saa kabla ya muda wa Mtihani na watakochelewa kwa zaidi ya nusu saa baada ya Mtihani kuanza hawataruhusiwa.
  - (b) Kufuata maelekezo yote yatakayotolewa na wasimamizi wa Mtihani.
  - (c) Kuandika namba ya Mtihani kwa usahihi.
  - (d) Kuhakikisha namba iliyoandikwa kwenye msimbomilia na namba ya Mtihani zinafanana.
  - (e) Kutofanya mawasiliano ya maneno au kwa njia yoyote baina ya watahiniwa. Ikiwa watahiniwa ana tatizo anatakiwa kunyoosha mkono ili kuomba msaada kwa msimamizi wa Mtihani.
  - (f) Watakojihusisha au watakoifanya udanganyifu watafutiwa matokeo yao ya Mtihani.